TANZANIA REVENUE AUTHORITY

KODI NA USHURU MBALIMBALI 2020/2021

Julai, 2020

DI NA USHURU 2020-2021_fnl.indd 1 7/14/20 9:19 A

	A : KODI YA MAPATO	VIWANGO	
Na.	MAELEZO	WAKAZI	WASIO WAKAZI
1.0	**Kodi ya Kampuni:**		
(a)	Kodi kwenye mapato yote ya kampuni	30%	30%
(b)	Makampuni yanayopata hasara kwa miaka 3 mfululizo. Isipokuwa kampuni zinazofanya shughuli za kilimo, afya na elimu.	0.5% ya mauzo ya mwaka	Hakuna
(c)	Kampuni mpya iliyoandikishwa katika soko la mitaji la Dar es Salaam yenye Umiliki wa usawa kwa umma kufikia 30% au zaidi katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo ya mwanzo.	25%	25%
(d)	Kampuni mpya iliyoanzishwa kwa ajili ya mitambo na mashine ya kuunganisha magari, matrekta na boti za uvuvi na injini za nje ya boti yenye Makubaliano ya kiutendaji na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Kipindi cha miaka 5 ya mwanzo tangu kuanza uzalishaji.	10%	Hakuna
(e)	Makampuni mapya ya viwanda vya madawa ya binadamu na viwanda vinavyotengeneza bidhaa za ngozi, yenye mkataba wa makubaliano na serikali ya Tanzania, yatapata punguzo la kodi ya mapato kwa miaka mitano ya mwanzo tangu kuanza uzalishaji.	20%	Hakuna
(f)	Makampuni ya viwanda vya kutengeneza taulo za kike (sanitary pads), yenye Mkataba wa Makubaliano na Serikali ya Tanzania yatapata punguzo la kodi ya mapato kwa miaka miwili mfululizo kuanzia tarehe 1.7.2019 hadi 30.6.2021	25%	Hakuna
(g)	Kodi kwenye mapato ya Tawi la Kampuni ya nje ya nchi lenye ukazi wa muda mrefu.	Hakuna	30%
(h)	Kodi kwenye mapato yanayorejeshwa nje ya nchi na tawi linalomilikiwa na mtu asiye mkazi.	Hakuna	10%

DI NA USHURU 2020-2021_fnl.indd 2 7/14/20 9:19 A

2.0	Kodi za zuio:		
(a)	(i). Gawio la hisa kutoka kampuni zilizoandikishwa kwenye soko la hisa la Dar-es-Salaam.	5%	5%
	(ii). Gawio la hisa kutoka Kampuni mkazi kwenda kampuni nyingine mkazi ambayo inamiliki hisa 25% au zaidi.	5%	Hakuna
(b)	Gawio la hisa kutoka kwenye makampuni mengine	10%	10%
(c)	Malipo ya kamisheni kwa wakala kwa kutuma fedha kwa njia ya simu za mkononi	10%	Hakuna
(d)	Ada, malipo mengine na malipo ya kamisheni kwa wakala shughuli za benki na malipo ya mtandao (Digital Payment)	10%	Hakuna
(e)	Riba	10%	10%
(f)	Mrahaba	15%	15%
(g)	Huduma za kiutawala na Kiufundi (Uchimbaji madini, mafuta na gesi)	5%	15%
(h)	Usafirishaji (Ndege za kukodi kwa wasio na makazi)	Hakuna	5%
(i)	Kipato kutokana na ukodishaji Ardhi/majengo	10%	20%
	Ndege	10%	15%
	Mali zingine	Hakuna	15%
(j)	Usafirishaji nje ya nchi	Hakuna	5%
(k)	Ada ya bima	Hakuna	5%
(l)	Ada itokanayo na maliasili	15%	15%
(m)	Ada ya huduma	5%	15%
(n)	Ada za wakurugenzi (Wakurugenzi wasio wa muda wote)	15%	15%
(o)	Malipo ya bidhaa yaliyouzwa kwa shirika mkazi na mtu yeyote	2% mauzo ghafi	Hakuna
(p)	Aina nyingine za kodi ya zuio	15%	15%

DI NA USHURU 2020-2021_fnl.indd 3 7/14/20 9:19 A

3.0	**Pato litokanalo na uuzaji wa rasilimali**		
	Pato kutokana na uuzaji hisa, ardhi na majengo (Mtu binafsi au kampuni)	10%	20%
	Misamaha katika mauzo ya rasilimali:		
	a) Makazi binafsi Pato la shilingi milioni 15 au pungufu. **b) Ardhi kwa ajili ya kilimo** Thamani ya soko chini ya shilingi milioni 10. **c) Hisa** Hisa zilizoorodheshwa kwenye soko la hisa la Dar-es-Salaam zinazomilikiwa na mkazi au asiye mkazi kwa kiwango kisichozidi 25%.		
4.0	**Mapato ya mkupuo mmoja**		
(a)	Usafirishaji nje ya nchi (Kwa wasio wakazi na wakodishaji wa ndege wasio na makazi maalum nchini)	Hakuna	5%
(b)	**Msamaha:** Mapato ya mkupuo mmoja yanayotokana na usafirishaji wa samaki, usafirishaji wa maua na mboga kwa ndege ya kigeni.		

Zingatia yafuatayo:

(i) **Kodi ya zuio** Kodi ya zuio hulipwa ndani ya siku 7 baada ya kila mwisho wa mwezi wa makato.

(ii) Ukokotoaji na malipo ya kodi ya zuio ni kwa njia ya mtandao ***www.tra.go.tz***

(ii) Ritani ya Kodi ya zuio huwasilishwa TRA ndani ya siku 30 kila baada ya kipindi cha miezi sita.

DI NA USHURU 2020-2021_fnl.indd 4 7/14/20 9:19 A

5.0	Kodi ya Mapato ya mtu binafsi (Tanzania Bara) kuanzia Julai, 2020	
	Mapato kwa Mwezi	**Kiwango cha Kodi**
	Mapato yasiyozidi Sh.270,000	Hakuna Kodi
	Mapato yanayozidi Sh.270,000 lakini hayazidi Sh. 520,000	9% ya mapato yanayozidi sh. 270,000
	Mapato yanayozidi Sh. 520,000 lakini hayazidi Sh. 760,000	Sh.22,500 + 20% ya mapato yanayozidi Sh.520,000
	Mapato yanayozidi Sh. 760,000 lakini hayazidi Sh. 1,000,000	Sh.70,500 + 25% ya mapato yanayozidi Sh760,000
	Mapato yanayozidi Sh.1,000,000	Sh.130,500 + 30% ya mapato yanayozidi Sh. 1,000,000
	Zingatia Kiwango cha mwaka: Mapato yasiyozidi Sh.3,240,000 hayatozwi kodi.	

5.1 Viwango vya kodi ya mapato kwa watu binafsi wakazi (Zanzibar) kuanzia tarehe 1 Aprili, 2017.

Mapato kwa Mwezi	Kiwango cha Kodi
Mapato yasiyozidi sh. 180,000	Hakuna Kodi
Mapato yanayozidi sh 180,000 lakini hayazidi sh. 360,000	9% ya mapato yanayozidi sh. 180,000
Mapato yanayozidi sh.360,000 lakini hayazidi sh. 540,000	sh.16,200 + 20% ya mapato yanayozidi sh.360,000
Mapato yanayozidi sh. 540,000 lakini hayazidi sh. 720,000	sh. 52,200 + 25% ya mapato yanayozidi sh. 540,000
Mapato yanayozidi sh.720,000	sh. 97,200 + 30% ya mapato yanayozidi sh. 720,000
Kiwango cha mwaka: Mapato yasiyozidi sh. 2,160,000/= hayatozwi kodi.	

DI NA USHURU 2020-2021_fnl.indd 5 7/14/20 9:19 A

Zingatia yafuatayo:

1. Wafanyakazi wanaochangia kulingana na kifungu namba 12 cha Sheria ya Mfuko wa Elimu ya mwaka 2001, mchango huo unaweza kusamehewa kodi endapo maombi yatatumwa kwa Kamishna.
2. (i) Kwa wafanyakazi wasio wakazi walio ajiriwa na mwajiri mkazi, mapato yao hutozwa kodi ya zuio ya 15%.
   (ii) Jumla ya mapato yapatikanayo nchini kwa mtu binafsi asiye mkazi hutozwa kodi kwa kiwango cha 30%
3. Mapato ya mwezi ni pamoja na mshahara, malipo kwa kazi za ziada,bonasi, kamisheni, na marupurupu mengine yatokanayo na ajira
4. Wafanyakazi wakazi na wasiowakazi wenye ajira ya ziada watakatwa Kodi ya zuio itokanayo na ajira ya ziada kiwango cha 30%

5.2	**Kodi kwenye marupurupu ya ajira**		
(a)	**Nyumba:** Ukokotoaji wa marupurupu ya mwajiriwa kutokana na nyumba aliyopewa na mwajiri yatazingatia bei ambayo ni ndogo kati ya bei ya soko na ile inayozidi yafuatayo: i. 15% ya mapato yote ya ajira ya mwaka ya mwajiriwa na ii. Madai ya marejesho yanayodaiwa na mwajiri kutokana na kodi ya pango		
(b)	**Gari:** Magari yatatozwa kodi kutokana na uwezo wa injini ya gari na umri wa gari kulingana na jedwali lifuatalo:		
	Uwezo wa injini ya gari	**Lisilozidi miaka mitano**	**Linalozidi miaka mitano**
(i)	Usiozidi 1000c.c	250,000/=	125,000/=
(ii)	Unaozidi 1000c.c na usiozidi 2000c.c	500,000/=	250,000/=
(iii)	Unaozidi 2000c.c na usiozidi 3000c.c	1,000,000/=	500,000/=
(iv)	Unaozidi 3000c.c	1,500,000/=	750,000/=

DI NA USHURU 2020-2021_fnl.indd 6 7/14/20 9:19 A

Zingatia

- Marupurupu haya hayatozwi kodi pale ambapo mwajiri hana madai ya makato kutokana na umiliki, matengenezo au matumizi ya gari.
- Bei ya soko itatumika kukadiria marupurupu ya aina nyingine.
- **Malipo ya mwezi ya mapato yatokanayo na Ajira (PAYE)** Huwasilishwa ndani ya siku saba baada ya mwisho wa mwezi wa malipo ya mshahara husika kuisha.
- **Ritani ya miezi sita ya mapato yatokanayo na Ajira (PAYE)** Mwaajiri anapaswa kujaza na kuwasilisha TRA Ritani ya mapato yatokanayo na Ajira ndani ya siku 30 baada ya miezi 6 ya Kalenda ya mwaka kuisha.

6.0	Tozo ya mafunzo na maendeleo ya ufundi stadi (SDL)
	i) Tanzania Bara kiwango ni 4 % ya malipo yote aliyolipa mwajiri kwa wafanyakazi wake kwa mwezi husika. ii) Tanzania Zanzibar kiwango ni 5%. **TAASISI ZINAZOSAMEHEWA SDL** a) Idara au Taasisi za Serikali ambazo zinaendeshwa kwa ruzuku ya Serikali b) Ofisi za Kidiplomasia c) Umoja wa Mataifa na Taasisi zake d) Taasisi za Kimataifa na Taasisi za Nje zinazotoa misaada ambazo hazijihusishi na biashara kwa namna yoyote ile. e) Taasisi za dini ambazo waajiriwa wake wameajiriwa kwa ajili ya kuendesha sehemu za kuabudu, kutoa mafunzo ya dini na kuelimisha dini kwa ujumla. f) Mashirika yanayotoa misaada ya hiari yasiyojihusisha na biashara kwa namna yoyote ile g) Serikali za Mitaa h) Mwajiri wa shamba ambaye waajiriwa wanajihusisha moja kwa moja na shughuli za kilimo pekee i) Taasisi na Vyuo vya Elimu vilivyosajiliwa ikijumuisha Shule za awali, za Msingi na Sekondari, Shule za mafunzo ya Ufundi Stadi, Vyuo Vikuu na Taasisi za Elimu ya Juu.

DI NA USHURU 2020-2021_fnl.indd 7 7/14/20 9:19 A

Zingatia

- Jumla ya malipo ni majumuisho ya mshahara, malipo ya likizo, likizo ya ugonjwa, malipo yoyote yanayo husiana na likizo, kamisheni, mafao, bonasi, malipo ya kujikimu, usafiri, malipo ya kujiburudisha au malipo yoyote yanayoendana na utendaji kazi husika isipokuwa malipo yale yaliyotumika katika utekelezaji wa moja kwa moja wa kazi ya mwajiri.
- Msamaha kwa Zanzibar itahusishwa Taasisi/Idara zilizopo kipengele (a). (d) na (g).
- **Ritani ya mwezi ya malipo ya SDL**
  Huwasilishwa ndani ya siku saba baada ya mwisho wa mwezi wa malipo ya mshahara husika kuisha.
- **Ritani ya miezi sita ya SDL**
  Mwaajiri anapaswa kujaza na kuwasilisha TRA Ritani ya tozo ya mafunzo na maendeleo ya ufundi stadi ndani ya siku 30 baada ya miezi 6 ya kalenda ya mwaka kuisha.

7.0 Viwango vya kodi wafanyabiashara wadogo wakazi

Mauzo kwa mwaka	**Uzingatiaji wa kifungu cha 35 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi (Utunzaji wa kumbukumbu)**	
	Asiyetunza Kumbukumbu	**Anayetunza Kumbukumbu**
Mauzo yasiyozidi sh. 4,000,000/=	Hakuna	Hakuna
Mauzo yanayozidi sh. 4,000,000/= na hayazidi sh. 7,000,000/=	Sh.100,000/=	3% ya mauzo yanayozidi sh. 4,000,000/=
Mauzo yanayozidi Sh. 7,000,000/= na hayazidi sh.11,000,0000/=	Sh. 250,000/=	Sh. 90,000/= +3% ya mauzo yanayozidi Sh. 7,000,000/=
Mauzo yanayozidi Sh. 11,000,000/= na hayazidi Sh. 14,000,000/=	Sh. 450,000/=	Sh. 230,000/= + 3% ya mauzo yanayozidi Sh. 11,000,000/=
Mauzo yanayozidi Sh. 14,000,000/= na hayazidi Sh. 100,000,000/=	Haihusiki	Sh. 450,000/= + 3.5 % ya mauzo yanayozidi Sh. 14,000,000/=

DI NA USHURU 2020-2021_fnl.indd 8 7/14/20 9:19 A

	Zingatia 1. Kusajili wafanyabiashara wadogo na watoa huduma kwenye sekta isiyo rasmi watatambuliwa na kupewa vitambulisho ambao mauzo ghafi hayazidi Sh. 4,000,000/= kwa mwaka. 2. Endapo mauzo ghafi kwa mwaka yanazidi Sh. 100,000,000/= ni lazima kutengeneza hesabu za mizania kulinganana biashara.
	3. Mlipakodi ambaye mauzo ghafi kwa mwaka yanazidi Sh.14,000,000/= anatakiwa kununua na kutumia mashine za kielektroniki za kodi (EFD). 4. Mlipakodi mwenye mauzo ghafi chini ya shilingi milioni 14 anatakiwa kutoa risiti ya kuandikwa kwa mkono zenye nakala zikionyesha jina la muuzaji, TIN yake, Jina la mnunuzi, aina ya bidhaa na thamani yake. ***Kifungu na. 36(3 & 4) cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi.***
7.1	**Uwasilishaji wa ritani na malipo ya kodi ya mapato.**
(a)	Tarehe za malipo ya kodi ya awali kwa walipakodi wanaofunga hesabu kwa kufuata mwaka wa kalenda i) Mnano au kabla tarehe 31 Machi ii) Mnano au kabla tarehe 30 Juni iii) Mnano au kabla tarehe 30 Septemba iv) Mnano au kabla tarehe 31 Disemba
(b)	**Angalizo***Malipo hufanyika katika kipindi cha miezi mitatu mitatu kutegemea tarehe ya kufunga hesabu za biashara. **Ritani za mwisho wa mwaka wa malipo ya kodi**: Huwasilishwa ndani ya miezi sita tangu tarehe ya kufunga hesabu za mwaka wa mapato.
(c)	**Riba kutokana na ucheleweshaji wa malipo:** Unaambatana na kutozwa riba kwa kiwango kilichoidhinishwa na Benki Kuu kwa wakati huo

DI NA USHURU 2020-2021_fnl.indd 9 7/14/20 9:19 A

(d)	**Kosa la kutokutoa risiti ya kodi ya kielektroniki (EFD)** (i) Mfanyabiashara atakayeshindwa kununua na kutumia mashine ya EFD; kushindwa kutoa risiti ya EFD, kutoa risiti ambayo ni ya uongo, kutumia mashine ya EFD kwa kupotosha mfumo na kumpotosha Kamishna au kuifanya mashine isifanye kazi au kutokutoa picha halisi atakuwa ametenda kosa kwa mujibu wa sheria na ikibainika atatozwa faini isiyopungua ***pointi za sarafu 200*** na zisizozidi ***pointi za sarafu 300*** au kifungo kisichozidi ***miaka 3 au vyote kwa pamoja.*** (ii) Mtu yeyote atakayebainika kuhusika katika makosa yaliyotajwa kifungu namba moja hapo juu ***atatozwa faini*** ambayo ni ***mara mbili ya kodi*** iliyokwepwa au kifungo kisichozidi ***miaka mitatu.*** (iii) Mtu yeyote atakayeshindwa kudai au kutoa taarifa ya kukataliwa ***kupewa risiti ya EFD*** au ***ankara ya malipo ya kielektroniki*** ya bidhaa au huduma atakuwa ametenda kosa na ikithibitika atatozwa faini isiyopungua ***pointi za sarafu 2*** na zisizozidi ***pointi za sarafu 100.*** ***(pointi ya sarafu 1 ni sawa na shilingi 15,000/=).***

8.0	**Uchakavu katika rasilimali na viwango vyake**	
Daraja	**Maelezo**	**Viwango**
1*	Kompyuta pamoja na vifaa vinavyohusiana na kompyuta, mashine zinazoshughulika na takwimu, vifaa/mashine zinazojiendesha zenyewe, mabasi makubwa na madogo yenye uwezo wa kubeba abiria wasiozidi 30, magari ya mizigo yanayobeba uzito sio chini ya tani 7, mashine nzito zinazotembea nchi kavu na zile zinazohusika na ujenzi.	37.5%

DI NA USHURU 2020-2021_fnl.indd 10 7/14/20 9:19 A

2*	Mabasi yenye uwezo wa kubeba abiria 30 au zaidi, magari makubwa kwa ajili ya kazi maalum, matrekta na matrekta yaliyojengewa makontena, reli, garimoshi na mashine zake, meli, matishari(barges), vyelezo(tags), na mashine nyingine zinazojiendesha zenyewe, mitambo na mashine zake pamoja na mashine ya upepo, jenereta za umeme, na mashine za usambazaji) zinazotumika katika uzalishaji au katika shughuli za madini, mitambo na mashine maalum kwa ajili ya matumizi ya jamii, na mashine au mitambo mingine kwa ajili ya umwagiliaji na mashine zake.	25%
3*	Samani za ofisini, vifaa vya ofisini na mashine/ mitambo, pamoja na rasilimali ambazo hazikujumuishwa kwenye madaraja mengine.	12.5%
5**	Majengo na sura mbali mbali za ujenzi, mabwawa, hifadhi ya maji, uzio, na shughuli nyingine za kilimo zenye asili ya kudumu kwa muda mrefu, shughuli za mifugo na uvuvi	20%
6**	Majengo, sura mbalimbali za ujenzi (structures), na shughuli nyingine zinazofanana na hizi zenye asili ya kudumu kwa muda mrefu ambazo hazipo katika daraja la 5.	5%
7**	Mali zisizoshikika.	Hugawanywa kwa muda wa maisha ya rasilimali.
8**	Mitambo na mashine (pamoja na mashine za upepo, jenereta za umeme, na mashine za usambazaji) zinazotumika kwenye kilimo, pamoja na mashine za kodi za kielektroniki (EFD) kwa wasio sajiliwa na VAT, Vifaa kwa matumizi ya utafutaji wa madini na mafuta.	100%
	Zingatia Gharama ya kukokotoa uchakavu wa magari yasiyo ya kibiashara, thamani ya kiasi kinachokubalika shilingi 30,000,000/= na kiasi kinachozidi hakitakubalika.	

DI NA USHURU 2020-2021_fnl.indd 11 7/14/20 9:19 A

8.1	**Punguzo la Uchakavu katika rasilimali katika shughuli za madini na mafuta**	
	Mwaka wa Mapato	**Kiwango cha uchakavu**
	Mwaka wa Kwanza	20% ya gharama
	Mwaka wa Pili	20% ya gharama
	Mwaka wa Tatu	20% ya gharama
	Mwaka wa Nne	20% ya gharama
	Mwaka wa Tano	20% ya gharama
	Zingatia* 1 Uchakavu hukokotolewa kwenye thamani ya rasilimali ambayo tayari imeshapunguzwa (Diminishing Value Method). ***Zingatia* 2**** Thamani ya rasilimali kwa mwaka wa kwanza ndio inayotumika katika kukokotoa uchakavu kila mwaka (Straight Line Method). ***Zingatia* 3** Daraja la 4 limefutwa kwa sheria ya fedha 2016.	
	B. KODI ZA MLAJI	
9.0	**KODI YA ONGEZEKO LA THAMANI (VAT)**	
	Usajili wa VAT • Kiwango cha usajili ni kwa mauzo yanayotozwa VAT cha zaidi ya shilingi milioni 100 kwa mwaka. **Usajili wa lazima** • Usajili wa huduma za kitaalamu zinazo stahili kutozwa VAT hufanyika bila kujali mauzo ya huduma kwa mwaka • Serikali na Taasisi zake zinazofanya shughuli za kiuchumi za kujipatia kipato nje ya kazi zao za msingi. • Kamishna Mkuu anaweza kumsajili mtu anayekusudia (Intending Trader) kutoza VAT kama atakidhi vigezo vya kisheria	

DI NA USHURU 2020-2021_fnl.indd 12 7/14/20 9:19 A

Viwango vya VAT

Aina ya bidhaa na au huduma zinazohusika	Kiwango (VAT)
Bidhaa na huduma zinazotozwa kodi -Tanzania bara	18%
Uagizaji na uingizaji wa bidhaa na huduma toka nje kuingia Tanzania bara.	18%
Uuzaji wa bidhaa nje ya nchi.	0%
Kutomhusisha mpitishaji bidhaa kulipa VAT kwa gharama ya huduma ya usafirishaji wa bidhaa/mizigo iendayo nje ya nchi kupitia Tanzania Bara, huduma zinajumuisha:-	0%
(i) Huduma zinazohusiana moja kwa moja na bidhaa inayopitishwa kwenda nje ya nchi (ii) Bidhaa zilizohifadhiwa kwenye bandari, uwanja wa ndege au maeneo ya forodha kwa kipindi kisichozidi siku 30 zikisubiri kusafirishwa au kwa kipindi cha ziada ambacho Kamishna wa Forodha ataruhusu..	0%

Msamaha wa VAT

Bidhaa na huduma zilizosamehewa zimeorodheshwa katika jedwali la Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Sura na. 148 soma na Sheria ya Fedha 2020.

i). Madawa, vifaa tiba, mitambo na vifungashio vya madawa ya binadamu kwa viwanda vinavyozalisha madawa hapa nchini *(vifungashio hivyo vikiwa na machapisho ya majina ya kiwanda husika).*

ii). Virutubisho na vitamini vitakavyo sambazwa Serikalini.

iii). Miradi ya Serikali inayotekelezwa kwa mikopo ya kibiashara.

Pale ambapo kuna mkataba uliosainiwa na Serikali ya Tanzania na Taasisi ya Fedha au Bank ambayo ni muwakilishi wa Serikali nyingine aliyepewa dhamana na kuingia mkataba na kusimamia utekelezaji wa miradi husika.

iv). Msaada uliyo idhinishwa na Waziri wa Fedha wenye makubaliano kati ya Serikali za Mitaa na Wafadhili.

v). Msamaha kwenye bima ya kilimo cha mazao

DI NA USHURU 2020-2021_fnl.indd 13 7/14/20 9:19 A

	Usajili wa VAT Zanzibar • Kiwango cha usajili kwa mauzo yanayotozwa VAT ni kuanzia shilingi milioni 50 kwa mwaka.	
	Viwango vya VAT Zanzibar	
	Bidhaa na huduma zinazotozwa VAT	15%
	Uingizaji wa bidhaa na huduma toka nje kuingia Zanzibar.	15%
	Uuzaji wa bidhaa nje ya nchi.	0%
	Uwasilishaji wa Ritani ya VAT na malipo:	
	Ritani ya VAT kwa bidhaa au huduma zitolewazo hapa nchini, itawasilishwa siku ya 20 ya mwezi unaofuata mwezi wa biashara	
	Zingatia • Endapo siku ya tarehe 20 itaangukia Jumamosi, Jumapili au Sikukuu ritani ya VAT itawasilishwa siku ya kwanza ya kazi inayofuata Jumamosi, Jumapili au Sikukuu.	
	• VAT kwa bidhaa toka nje kutozwa pindi malipo ya Ushuru wa Forodha yanapolipwa	
	• Kila mfanyabiashara aliyesajiliwa na Kodi ya Ongezeko la Thamani anatakiwa kutumia mashine za kielektroniki za kutolea risiti (EFD) .	
10.	**Ushuru wa Stempu**	
	Maelezo	**Viwango**
	(i) Kuhamisha miliki	Asilimia moja (1%) ya thamani ya mauzo au sihia
	(ii) Ardhi kwa ajili ya kilimo	Sh. 500/=
	(iii) Hati za kisheria na mikataba	Miamala ya kibiashara na kisheria, ushuru wa stempu hutozwa katika viwango maalum.

DI NA USHURU 2020-2021_fnl.indd 14 7/14/20 9:19 A

Misamaha ya ushuru wa Stempu

- Risiti kwenye mauzo au huduma inayohusiana na biashara
- Kuhamisha umiliki wa mali (Assets) katika chombo maalum kwa madhumuni ya kutoa dhamana zinazotegemea mali hiyo.

Zingatia

Ushuru wa Stempu kwenye hati mbalimbali, unapaswa kulipwa ndani ya siku 30 baada ya kusaini mkataba husika.

11. Ushuru wa Forodha

Bidhaa	Kiwango cha Ushuru
(i) Bidhaa za Mtaji, Malighafi zitumikazo kuzalisha bidhaa, dawa na vifaa vya hospitali, Jembe la mkono, matrekta ya kilimo na pembejeo za kilimo.	0%
(ii) Bidhaa ambazo hazijakamilika	10%
(iii) Bidhaa za mlaji na zilizokamilika	25%

Baadhi ya bidhaa hutozwa ushuru zaidi ya 25% kwa lengo la kulinda viwanda vya ndani. Hii ni pamoja na :-

Maziwa yaliyosindikwa na bidhaa za aina hiyo, Maziwa ya mtindi na mafuta ya maziwa yaliyoongezwa ladha, Sukari itokanayo na miwa au viazi na bidhaa za aina hiyo, Magunia ya katani, Vitenge, Khanga na Nguo za mitumba.

12. Ushuru wa bidhaa

Ushuru wa bidhaa hutozwa kwa bidhaa maalum ambazo zina stahili kutozwa ili kulinda viwanda vya ndani na kuzuia Tanzania isiwe sehemu ya kutupa bidhaa zilizopitwa na wakati au ambazo hazifikii viwango vya ubora. Hakuna mabadiliko kwenye viwango maalum kwa mwaka huu wa fedha 2020.

Msamaha:

- Uingizaji wa vilainishi na mtoa huduma wa ndani ya nchi au mteule wa ndege wa kutoa huduma chini ya makubaliano kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya kigeni (Fedha, 2019).
- Misamaha mingine rejea jedwali la misamaha la sheria husika.

DI NA USHURU 2020-2021_fnl.indd 15 7/14/20 9:19 A

A. (i) Viwango maalum kwa bidhaa za:

Mvinyo, pombe kali, bia, vinywaji baridi, maji ya chupa, juisi za matunda, sigara, tumbaku, DVD, VCD, CD na kanda zilizorekodiwa, bidhaa za petroli na gesi.

(ii) Ushuru kwa asilimia ya thamani:

10%, 15%, 17%, 20%, 25% na 50% (15% kwa samani kutoka nje ya nchi.

(iii) Ushuru wa bidhaa kwa kwa bia na Juisi za unga:

- Bia za unga zenye HS Code 2106.90.99 zinazoingizwa nchini Sh. 844/= kwa kilo.
- Juisi za Unga zenye HS Code 2106.90.99 zinazoingizwa nchini Sh. 232/= kwa kilo.

Uwasilishaji wa ritani za kila mwezi:

Mtengenezaji yeyote wa bidhaa au mtoaji wa huduma zinazotozwa ushuru wa bidhaa anatakiwa kuwasilisha ritani ya kila mwezi mnamo au kabla siku ya mwisho ya kazi ya mwezi unaofuata mwezi wa malipo husika.

B. Ushuru wa bidhaa kwenye magari kulingana na ujazo wa injini kwa magari ya matumizi binafsi

	Aina ya gari	Kiwango cha ushuru
(i)	Lenye ujazo wa injini chini ya 1000cc	0%
(ii)	Lenye ujazo wa injini unaozidi 1000 cc lakini usiozidi 2000 cc	5%
(iii)	Lenye ujazo wa injini unaozidi 2000 cc	10%

C. Ushuru wa bidhaa wa ziada kwa magari yaliyotumika:

(i)	Magari madogo yenye umri wa kuanzia miaka 8 na isiyozidi 10, inayohesabiwa kuanzia mwaka gari ilipotengenezwa	15%
(ii)	Magari madogo yenye umri wa kuanzia miaka 10 na zaidi, inayohesabiwa kuanzia mwaka gari ilipotengenezwa **Zingatia** (i&ii) isipokuwa magari ya abiria kwenye HS Code 8702.10.22, 8702.10. 29, 8702.10.99, 8702.90.29 na 8702.90.99	30%

DI NA USHURU 2020-2021_fnl.indd 16 7/14/20 9:19 A

	D. Uingizaji wa vipuri vya magari vilivyotumika	
	Vipuri vya magari na pikipiki vilivyotumika vinatozwa ushuru wa bidhaa	25%
	E. Ushuru kwa bidhaa na huduma nyinginezo	
	Ada au tozo zinazolipwa kwa taasisi au makampuni ya mawasiliano kwa huduma ya kuhamisha fedha	10%
13.	**Ushuru wa mafuta: Hutozwa kwa lita**	Sh. 313/= kwa lita
14.	**Ushuru wa mafuta ya Taa, Gesi na spiriti**	Sh. 50/= kwa lita
15.	**Tozo ya kuendeleza Utalii:** hutozwa katika gharama ya malazi	Dola ya Kimarekani 1.5 kwa usiku
16.	**Tozo ya kuendeleza Reli** hutozwa katika gharama ya kiforodha ya kuingiza bidhaa	1.5% ya gharama (CIF)
	Zingatia Tozo hii haitatozwa kwa vitu vilivyosamehewa chini ya Sheria ya Forodha ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004, na vitu vilivyosamehewa katika jedwali la tano la sheria husika isipokuwa bidhaa na vifaa vya famasia sura ya 30 na 90 na mbolea kama ilivyotafisiriwa chini ya sheria ya viwango vya ushuru wa pamoja ya Afrika mashariki.	
17.	**Ushuru wa huduma za Viwanja vya Ndege**	
	Safari za ndani ya nchi	Sh. 10,000/-
	Safari za nje	Dola za kimarekani 40
	Uwasilishaji wa Ritani: Ritani kwa huduma itawasilishwa mnamo au kabla ya siku ya mwisho ya kazi ya mwezi unaofuata mwezi wa biashara	
18.	**Ada za huduma ya Bandari**	
	Kwa wasafiri wakazi	Sh. 500/-
	Kwa wageni wasio wakazi	Dola za kimarekani 5
	Uwasilishaji wa Ritani: Ritani kwa huduma itawasilishwa mnamo au kabla ya siku ya mwisho ya kazi ya mwezi unaofuata mwezi wa biashara	

DI NA USHURU 2020-2021_fnl.indd 17 7/14/20 9:19 A

19.	**Ada ya usajili wa chombo cha moto kwa mara ya kwanza hutegemea uwezo wa injini ya gari (cc)**	
	Uwezo wa Injini (cc)	**Ada**
	501 – 1500cc	Sh.200,000/-
	1501 – 2500cc	Sh. 250,000/-
	2501 na zaidi	Sh. 300,000/-
	Ada ya kusajili pikipiki	Sh.95,000/-
	Ada ya usajili kwa namba Binafsi	Sh.10,000,000/- kwa miaka 3
	Ada ya usajili kwa kutumia namba maalumu ambayo ni nyongeza ya ada ya usajili wa gari	Sh. 500,000/=
20.	**Kuhamisha umiliki wa chombo cha moto**	
	Ada ya gari	Sh. 50,000/-
	Ada ya pikipiki	Sh. 27,000/-
	Ada ya Nakala ya kadi (Duplicate)	
	Gari	Sh. 50,000/=
	Pikipiki ya magurudumu matatu(Bajaj)	Sh. 30,000/=
	Pikipiki	Sh. 20,000/=.
21.	**Leseni za Udereva**	
	Ada ya leseni kila baada ya miaka mitano	Sh 70,000/-
	Ada ya majaribio ya udereva	Sh. 3,000/=
	Leseni ya muda ya udereva	Sh 10,000/-
22.	**Ushuru kwa bidhaa ziendazo nje ya nchi (Export Tax)**	
	i) Ngozi ghafi hutozwa 80% ya thamani (FOB) au Dola za kimarekani 0.52 kwa kilo kutegemea kiasi kipi ni kikubwa.	
	ii) Ngozi chepe bluu hutozwa 10% ya thamani (FOB)	
23.	**Udhibiti wa madini kusafirishwa nje ya nchi au kwa matumizi ya ndani**	
	Haitaruhusiwa kuondosha au kusababisha usafirishaji wa madini nje ya nchi au kwa matumizi ya ndani, hadi taratibu za kisheria zinapotimizwa.	

DI NA USHURU 2020-2021_fnl.indd 18 7/14/20 9:19 A

24.	**Tozo kwa Korosho zisizobanguliwa**
	Korosho zisizobanguliwa hutozwa ushuru wa 15% kwenye thamani (FOB) au dola za kimarekani 160 kwa tan**i** kutegemea kiwango kipi ni kikubwa
25.	**Bidhaa zisizoruhusiwa kuingia hapa nchini (Prohibited Goods)**
	Dawa za kulevya, Vifaa vya kutengeneza gesi za machozi, Maandishi ya uchochezi, Picha za matusi, matairi ya Magari ya kubeba abiria na biashara yaliyokwisha tumika na bidhaa zingine kama zilivyoainishwa katika sheria.
26.	**Bidhaa zisizoruhusiwa kuingia hapa nchini kwa masharti ya udhibiti (Restricted Goods)**
	Wanyama hai, mimea, baruti, silaha, risasi, pembe za ndovu na mabaki yake pamoja na bidhaa zingine kama zilivyoainishwa katika sheria.
	Bidhaa hizi zinahitaji kibali maalum kutoka Mamlaka au Taasisi husika.
27.	**Ada ya mchakato wa forodha (Processing Fee)**
	Ada ya 0.6% hutozwa kwa ajili ya mchakato wa kuandaa nyaraka za forodha kwa kutumia thamani ya bidhaa (FOB).
28.	**Bidhaa zinazotoka Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na SADC**
	Bidhaa zinazozalishwa katika nchi Wanachama wa EAC na SADC zitatozwa ushuru kiwango cha 0% pale zinapokidhi kanuni za uasili. Kiwango hiki hakitazihusu bidhaa zinazozalishwa katika uwanda wa wazi (EPZ) na viwanda vinavyopata msamaha wa kodi. Nchi Wanachama wa EAC ni Burundi, Kenya, Rwanda, Sudan ya Kusini, Tanzania, na Uganda.
	Zingatia: Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zinatekeleza mfumo wa Himaya moja ya forodha lengo ikiwa ni uondoaji wa vikwazo vya biashara na kupunguza udhibiti wa mpaka wa ndani kwa bidhaa zinazohamia ndani ya Nchi Wanachama.

DI NA USHURU 2020-2021_fnl.indd 19 7/14/20 9:19 A

29.	Maduhuli (Non tax revenue).

1. Kodi ya Majengo - Maeneo ya kutoza

(a) Majiji, Manispaa na Halmashauri za Miji.

(i) **Sh 10,000/=** kwa jengo kwa nyumba ya kawaida katika kiwanja chenye jengo moja linalotumika

(ii) **Sh 10,000/=** kwa kila jengo la nyumba ya kawaida linalotumika lililopo ndani ya kiwanja kimoja.(Mfano kama kuna nyumba zaidi ya moja kila moja itatozwa **Sh. 10,000/=)**

(iii) **Sh 50,000/=** kwa kila sakafu ya nyumba ya ghorofa kwa maeneo ya **Majiji, Manispaa na Halmashauri za Miji**

(b) Halmashauri za Wilaya

(i) **Sh10,000/=** kwa jengo kwa nyumba ya kawaida inayotumika.

(ii) Iwapo kiwanja kina nyumba zaidi ya moja basi jengo lenye thamani ya juu ndilo litakalohesabika na kutozwa **Sh. 10,000/=** tu.

(iii) **Sh 20,000/=** tu kwa nyumba ya ghorofa katika maeneo ya Wilaya.

Angalizo:

- Endapo jengo moja linamilikiwa na watu tofauti tofauti (Unit Titles) wenye Umiliki kila mmoja, atalipa kodi ya jengo kwa **sehemu ya jengo anayomiliki.**
- Halmashauri za Wilaya maeneo ya kutoza ni yale **yaliyoko ndani ya mipaka ya makao makuu ya Wilaya na Mamlaka za Miji tu.**
- Majengo yasiyotozwa kodi ni **Kibanda cha udongo, nyumba za nyasi na makuti na nyumba za matope au udongo** na zinazofanana nazo.

Malipo ya kodi ya majengo

- Mwisho wa kulipa kodi ya Majengo ya mwaka husika ni tarehe 31Disemba ya kila mwaka.

DI NA USHURU 2020-2021_fnl.indd 20 7/14/20 9:19 A

2. Ushuru wa Matangazo ya Biashara kwenye Mabango

Jedwali la Viwango

Na	Maelezo	Ada (kwa Sh.)
1.	Mabango yasiyo na mwanga	15,000/= kwa futi ya mraba
2.	Mabango yenye mwanga	18,000/= kwa futi ya mraba
3.	Mabango ya kwenye ukuta	15,000/= kwa futi ya mraba
4.	Mabango ya kielekitroniki	20,000/= kwa futi ya mraba
5.	Magari ya matangazo	15,000/= kwa futi ya mraba
6.	Magari yaliyobandikwa matangazo ya bidhaa wanazozalisha	4,000/= kwa futi ya mraba
7.	Matangazo kwenye kituo cha mauzo:	
	Mabango yasiyo na mwanga	15,000/= kwa futi ya mraba
	Mabango yenye mwanga	18,000/= kwa futi ya mraba
8.	Kila tangazo la biashara kwa matangazo ya awali 100	100,000/=
	Kwa kila tangazo jingine lenye matangazo ya jumla 100 au sehemu	55,000/=
9.	Matangazo ya biashara ya muda mfupi au ya promosheni kwa siku	55,000/=

DI NA USHURU 2020-2021_fnl.indd 21 7/14/20 9:19 A

Msamaha:
Matangazo ya Mabango yanayoelekeza sehemu Huduma za kijamii zinapopatikana kama shule, zahanati, hospitali.

3. Ushuru wa Bandari

TRA ilipewa jukumu la kukusanya ushuru wa bandari kuanzia tarehe 1 Agosti, 2016

4. Michezo ya kubahatisha

	A. Casino	**Viwango vya Kodi**	**Tarehe ya kulipa**
i)	Shughuli za Casino	18% ya mapato baada ya kuondoa gharama za washindi	Kila mwezi kabla ya tarehe 7 ya mwezi unaofuata
ii)	Casino ya Mitandaoni	25% ya mapato baada ya kuondoa gharama za washindi	Kila mwezi kabla ya tarehe 7 ya mwezi unaofuata
	Kodi kwa washindi		
i)	Kodi kwenye ushindi wa Casino	12% ya mapato ya Casino	Kila wiki kabla ya Jumatano
ii)	Kodi kwenye ushindi	20% kwa michezo yote isipokuwa michezo ya Casino	Kila mwezi kabla ya tarehe 7 ya mwezi unaofuata
B.	**Aina ya michezo mengine ya kubahatisha**		
1.	Michezo ya kubahatisha (Sports betting)	25% ya pato ghafi la mauzo	Kila mwezi kabla ya tarehe 7 ya mwezi unaofuata
2.	SMS	25% ya pato halisi la mchezo	Kila mwezi kabla ya tarehe 7 ya mwezi unaofuata

DI NA USHURU 2020-2021_fnl.indd 22 7/14/20 9:19 A

	3.	Michezo ya kubahatisha (Slot Machines)	Shillingi 100,000/= kwa kila machine	Kila mwezi kabla ya tarehe 7 ya mwezi unaofuata
	4.	Bahati Nasibu ya Taifa	20% ya mapato ghafi ya mchezo	Kila mwezi kabla ya tarehe 7 ya mwezi unaofuata
	5.	Mashine arobaini	25% ya pato halisi	Kila mwezi kabla ya tarehe 7 ya mwezi unaofuata

5. Tozo, Ada, Mapato au malipo toka Sekta ya Utalii.

TRA imepewa jukumu la kukusanya Tozo, Ada, Mapato au Malipo kutoka Sekta ya Utalii kuanzia tarehe 1 Julai 2020.

30. Malipo ya marejesho ya kodi.

- Kamishna atatathmini na kuamua kufanya marejesho au kutokufanya ndani ya siku 90 baada ya kupokea maombi yaliyokamilika.
- Kamishna atalipa marejesho ya kodi ndani ya siku 14 tangu tarehe ya kufanya uamuzi.
- Maombi ya marejesho ya kodi iliyolipwa kwa ziada yanatakiwa kufanyika ndani ya miaka mitatu tangu tarehe ya malipo ya kodi iliyolipwa kwa ziada.

31. Sheria ya Usimamizi wa Kodi

(i) Marekebisho yanayohusu usajili wa TIN kifungu cha 22

- Iwapo mtu amesajiliwa na kupewa Namba ya Utambulisho wa Mlipakodi (TIN) kwa ajili ya biashara au uwekezaji kwa mara ya kwanza, kiasi cha kodi ya mapato kitakachokadiriwa kitaahirishwa kwa kipindi cha miezi sita tangu tarehe ya kupata TIN
- Mlipakodi aliyeahirishiwa kodi atapaswa kulipa kiasi kilichoahirishwa kwa awamu tatu ndani ya mwaka husika wa mapato

DI NA USHURU 2020-2021_fnl.indd 23 7/14/20 9:19 A

- Endapo kodi iliyoahirishwa itapelekea kuvuka mwaka wa mapato husika, mlipakodi atalazimika kulipa kiasi chote cha kodi katika awamu ya mwisho ya mwaka wa mapato husika.
- Mlipakodi hatazuiwa kulipa kodi ya mapato aliyokadiriwa katika kipindi kilichoahirishwa endapo ataamua kulipa kwa hiari yake .

(ii) Usaliji wa wafanyabiashara wadogo na watoa huduma *kifungu cha 22 A*

- Wafanyabiashara wote wadogo wakazi ambao mauzo yao kwa mwaka yanazidi shillingi 4,000,000/= kwa mwaka wanatakiwa kujisajili na kupata TIN.

(iii) Uwakilishi kwenye masuala yote ya kikodi

kifungu cha 27

- Sheria imetaja wawakilishi wa walipakodi ambao ni Wakili, Mshauri wa kodi au mtu mwingine aliye idhinishwa kwa taratibu za kisheria na Mlipakodi mwenyewe.

(vi) Ukomo wa kuwasilisha taarifa kwa Kamishna Mkuu *kifungu cha 44*

- Sheria imeweka ukomo kwa walipakodi kuwasilisha taarifa kwa kamishna mkuu ili kuharakisha utoaji wa maamuzi ya kikodi.
- Sheria imeweka ukomo wa miezi 6 wa Kamishna Mkuu kushughulikia utatuzi wa mapingamizi ya kodi.

MUHIMU KUZINGATIA

Tunza kumbukumbu sahihi za biashara yako
Wasiliana na Maafisa wa TRA ofisi iliyo karibu nawe kwa ufafanuzi wa sheria za kodi.
Toa taarifa iwapo mwenendo wa biashara yako itakapo badilika (Kusimama, Kufunga, Kukua na kuongeza tawi jengine la biashara)
Tundika TIN eneo la wazi la biashara yako
TRA ipo kukuhudumia
Pata TIN mtandaoni (Online)
Lipa kodi kiganjani mwako
Epuka matapeli toa taarifa TRA

DI NA USHURU 2020-2021_fnl.indd 24 7/14/20 9:19 A